

## **MADIWANI WA MOROGORO WAOMBWA KUSISITIZA KUHUSU MAZINGIRA, CHAKULA MASHULENI NA KUTOA TAARIFA ZA UHALIFU**

Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro wametakiwa kuIsisitiza jamii kuhusu mpango wa chakula cha mchana mashuleni, utunzaji wa mazingira na kutoa taarifa za uhalifu mara unapojitokeza ndani ya kata zao.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mheshimiwa Rebecca Nsemwa alipokuwa akitoa salamu za Wilaya wakati wa Kikao cha Mikutano wa Kawaida wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro uliofanyika jana tarehe 03.08.2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa hiyo.



"Ninawaomba Waheshimiwa Madiwani muwapo kwenye Kata zenu sisitizeni wananchi kuhusu mpango wa chakula cha mchana mashuleni kwa sababu watoto wakipata chakula cha mchana mashuleni inaweza kusaidia kuongeza kiwango cha ufaulu na kuimarisha afya zao. Lingine ninalowaomba ni kwamba msiache kuzungumzia suala la uharibifu wa mazingira kwa sababu mazingira yanapoharibiwa mvua zitakuwa haba na umeme vilevile. Pia ninawaomba msiache kutoa taarifa za uhalifu pindi unapojitokeza ndani ya Kata zenu kwa sababu kiwango cha uhalifu kikiwa juu Manispaa inaweza kukawia kuwa jiji lakini pia Serikali yetu inachafuka na kuonekana haisimamii vyema usalama wa raia wake jambo ambalo sio sahihi" alieleza kwa kina Mheshimiwa Nsemwa.



Vilevile, Mheshimiwa Nsemwa amewataka waheshimiwa Madiwani kushirikiana na Ofisi yake kuhakikisha wanatatua suala la magari madogo ya abiria, maarufu kama daladala kutotumia vizuri Stendi ya Magari Madogo, ya Mafiga ambayo imejengwa kwa gharama kubwa lakini mpaka sasa haiingizi mapato kwa Manispaa kwa sababu haitumiki ipasavyo.

"Ndugu zangu, tukitaka mambo endelevu ni lazima tuchukue hatua hata hatua hizo zitawakera watu kwa sasa lakini baadae wataelewa na wote kwa pamoja tutafurahia matunda yake. Ofisi yangu tunataka kuandaa upya ruti za magari ya abiria na ni lazima tutengeneze ruti ndefu ili magari hayo yalazimike kupita Mafiga ili kukamilisha ruti zake. Ninawaomba tushirikiane katika hili kwa kuwaeleimisha wananchi wetu ili ruti hizi zitakapoanza zilete mafaniko na stendi yetu ya Mafiga iweze kuingiza mapato kusudiwa dani ya Manispaa yetu" alifafanua Mheshimiwa Nsemwa.



Aidha, Mheshimiwa Nsemwa amewapongeza Watendaji na Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro kwa kazi nzuri wanazozifanya ikiwemo ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 uliokwisha Juni, 2023, Manispaa ya Morogoro ilifanikiwa kukusanya fedha za Mapato ya Ndani shilingi bilioni 13, sawa na asilimia 109 ya makusanyo yake.

#### **MWISHO**